# ELIMU YA KILIMO BORA CHA PAMBA YAWAFIKIA WANAITILIMA

**Serikali ya Wilaya ya Itilima Mkoani Simiyu kwa kushirikiana Bodi ya Pamba imeendelea na utoaji wa elimu kwa wakulima juu ya kilimo cha kisasa ambacho kitaleta tija, ilikuweza kuongeza kasi ya uzalishaji wa zao hilo pamoja na kipato kwa wakulima ili kuweza kuondokana na umasikini.**

Kupitia Balozi wa Pamba Tanzania Mh: **Aggrey Mwanri** pamoja na timu ya Wataalamu kutoka Bodi ya Pamba, Mkoa pamoja na Wilaya wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima **Bi. Elizabeth Gumbo** wamefanikiwa kuwafikia wakulima katika vijiji mbalimbali na kuwapatia elimu juu ya kilimo bora na chenye tija cha cha pamba.

Akiwa katika kata ya Mwamapalala Mhe Mwanri aliuliza **"kama wenzetu kutoka Mataifa ya Brazil, Argentina na Misri wanavuna kilo kuanzia 1800 – 2000 kwa eka moja kwa nini sisi tubaki katika uzalishaji wa kilo 150 – 200 kwa eka?"**

Aidha Mhe. Mwanri aliwataka Wakuliwa Waitilima na Simiyu kwa ujumla kuachana na kilimo cha mazoea ambacho hakina tija, ili kufikia lengo la Mkoa la kuzalisha **tani 500,000** na katika hili wakulima wanapaswa kufuata kanuni za kilimo bora ambacho mkulia atatakiwa kutumia vipimo vya **sentimita 30** kutoka mche hadi mche na **sentimita 60** kutoka mstari hadi mstari na kwa utaratibu huu Mkulima atakuwa na uwezo wa kuotesha **miche 44,444** kwa eka moja badala ya **miche 22,222** kwa eka moja.

Vilevile **Mwanri** alihamasisha matumizi ya mbolea za asili (samadi) kwani mbolea hiyo hurutubisha udongo, huhifadhi unyevunyevu, pamoja kutunza uhai wa ardhi Kwa mda mrefu zaidi, pia amewataka wakulima kuhakikisha wanaondoa masalia pamoja na maotea ya mazao Kwa kuyachoma moto baada ya mavuno njia hii husaidia kupambana na wadudu hatari wa zao la pamba kama Funza, Chawageni na Kangambili.

Balozi huyo wapamba alizungumzia namna bora ya matumizi ya viwatilifu vya kuulia wadudu, kwa lengo la mkulima kupata matokeo mazuri, matumizi ya viwatilifu yaje baada ya kujiridhisha kuwa shamba limevamiwa na wadudu na upuliziaji ufuate utaratibu wa maelekezo ya wataalamu kama kupima mwelekeo wa upepo, kujihifadhi vizuri ili dawa isimuathiri mkulima na upuliziaji usifanyike kama kunadalili za mvua au kuwepo kwa umande.

Scanned with CamScanner

Kwa upande wa Palizi **Mhe. Mwanri** alisisitiza na kuonyesha kwa vitendo palizi sahihi na palizi ambalo sio sahihi, palizi sahihi uambatana kuuzogezea mmea Udongo na kuondoa magugu yasiyo hitajika huku ukiilinda mizizi ya mmea husika lakini palizi mbovu niile ya kuondoa udongo katika mmea na mizizi ya mmea husika ikiwa wazi hali hii hudumaza ukuaji wa mmea.

Akizungumzia suala la uvunaji Mhe. Mwanri alitahadharisha wakulima kujiadhari na uvunaji ambao sio sahihi unao huusisha uchukuaji wa pamba haraka haraka na kupelekea kuichanganya pamba na magome pamoja na majani hii husababisha pamba kuwa chafu na kukosa thamani halisi, na alizuia uwekaji wapamba katika mifuko ya sandarusi ambapo hupelekea pamba kubaki na nyuzinyuzi za plastiki.

Kwa kuhitimisha mafunzo hayo **Balozi Aggrey Mwanri** aliwaapisha wanasemina wote kwa lengo la kuwataka wakatekeleze kwa vitendo kanuni na taratibu zote zinazoongoza zao la pamba pamoja kuitekeleza **sheria Namba 2 ya mwaka 2001** inayo ipa serikali kupitia Bodi ya Pamba jukumu la kusimamia zao la pamba na hatimaye kuongeza uzalishaji na pato la mkulima.

Kwaupande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (W) Itilima Bi**: Elizabeth Gumbo** aliwahimiza wakulima wilayani humo, kuhakikisha wanazingatia Elimu inayotolewa na wataalam, iliwaweze kupata uzalishaji mkubwa utakao wanufaisha zaidi na kufanya uchumi wao kukua.

Akiwakilisha Wananchi wa Kata ya Mwamapalala, Diwani wa kata hiyo Mhe. **Emmanuel Lugisa** ametoa shukurani kwa serikali ya mkoa wa Simiyu kwa kutoa elimu ambayo itaewasaidia wakulima kupata ujuzi, Vilevile amewataka maafisa kilimo waendele kutoa mafunzo kupitia shamba darasa kwa kila kata na vijiji vyake huku akisisitiza Maafisa wa Bodi ya Pamba kuleta Mbegu na Viwatilifu kwa wakati mwafaka

**Mkoa wa simiyu unazalisha asilimia 60 (%) za Pamba yote inayolimwa Nchini na kwa msimu wa mwaka 2021-2022 Mkoa umejiwekea malengo ya kuzalisha tani 500,000 ambapo Wilaya ya Itilima ikiwa na jukumu la kuzalisha tani 70,000 za Pamba.**

.

## HITIMISHO

Scanned with CamScanner

# ELIMU YA KILIMO BORA CHA PAMBA YAWAFIKIA WANAITILIMA

**Serikali ya Wilaya ya Itilima Mkoani Simiyu kwa kushirikiana Bodi ya Pamba imeendelea na utoaji wa elimu kwa wakulima juu ya kilimo cha kisasa ambacho kitaleta tija, ilikuweza kuongeza kasi ya uzalishaji wa zao hilo pamoja na kipato kwa wakulima ili kuweza kuondokana na umasikini.**

Kupitia Balozi wa Pamba Tanzania Mh: **Aggrey Mwanri** pamoja na timu ya Wataalamu kutoka Bodi ya Pamba, Mkoa pamoja na Wilaya wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima **Bi. Elizabeth Gumbo** wamefanikiwa kuwafikia wakulima katika vijiji mbalimbali na kuwapatia elimu juu ya kilimo bora na chenye tija cha cha pamba.

Akiwa katika kata ya Mwamapalala Mhe Mwanri aliuliza **"kama wenzetu kutoka Mataifa ya Brazil, Argentina na Misri wanavuna kilo kuanzia 1800 – 2000 kwa eka moja kwa nini sisi tubaki katika uzalishaji wa kilo 150 – 200 kwa eka?"**

Aidha Mhe. Mwanri aliwataka Wakuliwa Waitilima na Simiyu kwa ujumla kuachana na kilimo cha mazoea ambacho hakina tija, ili kufikia lengo la Mkoa la kuzalisha **tani 500,000** na katika hili wakulima wanapaswa kufuata kanuni za kilimo bora ambacho mkulia atatakiwa kutumia vipimo vya **sentimita 30** kutoka mche hadi mche na **sentimita 60** kutoka mstari hadi mstari na kwa utaratibu huu Mkulima atakuwa na uwezo wa kuotesha **miche 44,444** kwa eka moja badala ya **miche 22,222** kwa eka moja.

Vilevile **Mwanri** alihamasisha matumizi ya mbolea za asili (samadi) kwani mbolea hiyo hurutubisha udongo, huhifadhi unyevunyevu, pamoja kutunza uhai wa ardhi Kwa mda mrefu zaidi, pia amewataka wakulima kuhakikisha wanaondoa masalia pamoja na maotea ya mazao Kwa kuyachoma moto baada ya mavuno njia hii husaidia kupambana na wadudu hatari wa zao la pamba kama Funza, Chawageni na Kangambili.

Balozi huyo wapamba alizungumzia namna bora ya matumizi ya viwatilifu vya kuulia wadudu, kwa lengo la mkulima kupata matokeo mazuri, matumizi ya viwatilifu yaje baada ya kujiridhisha kuwa shamba limevamiwa na wadudu na upuliziaji ufuate utaratibu wa maelekezo ya wataalamu kama kupima mwelekeo wa upepo, kujihifadhi vizuri ili dawa isimuathiri mkulima na upuliziaji usifanyike kama kunadalili za mvua au kuwepo kwa umande.

Scanned with CamScanner

Kwa upande wa Palizi **Mhe. Mwanri** alisisitiza na kuonyesha kwa vitendo palizi sahihi na palizi ambalo sio sahihi, palizi sahihi uambatana kuuzogezea mmea Udongo na kuondoa magugu yasiyo hitajika huku ukiilinda mizizi ya mmea husika lakini palizi mbovu niile ya kuondoa udongo katika mmea na mizizi ya mmea husika ikiwa wazi hali hii hudumaza ukuaji wa mmea.

Akizungumzia suala la uvunaji Mhe. Mwanri alitahadharisha wakulima kujiadhari na uvunaji ambao sio sahihi unao huusisha uchukuaji wa pamba haraka haraka na kupelekea kuichanganya pamba na magome pamoja na majani hii husababisha pamba kuwa chafu na kukosa thamani halisi, na alizuia uwekaji wapamba katika mifuko ya sandarusi ambapo hupelekea pamba kubaki na nyuzinyuzi za plastiki.

Kwa kuhitimisha mafunzo hayo **Balozi Aggrey Mwanri** aliwaapisha wanasemina wote kwa lengo la kuwataka wakatekeleze kwa vitendo kanuni na taratibu zote zinazoongoza zao la pamba pamoja kuitekeleza **sheria Namba 2 ya mwaka 2001** inayo ipa serikali kupitia Bodi ya Pamba jukumu la kusimamia zao la pamba na hatimaye kuongeza uzalishaji na pato la mkulima.

Kwaupande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (W) Itilima Bi**: Elizabeth Gumbo** aliwahimiza wakulima wilayani humo, kuhakikisha wanazingatia Elimu inayotolewa na wataalam, iliwaweze kupata uzalishaji mkubwa utakao wanufaisha zaidi na kufanya uchumi wao kukua.

Akiwakilisha Wananchi wa Kata ya Mwamapalala, Diwani wa kata hiyo Mhe. **Emmanuel Lugisa** ametoa shukurani kwa serikali ya mkoa wa Simiyu kwa kutoa elimu ambayo itaewasaidia wakulima kupata ujuzi, Vilevile amewataka maafisa kilimo waendele kutoa mafunzo kupitia shamba darasa kwa kila kata na vijiji vyake huku akisisitiza Maafisa wa Bodi ya Pamba kuleta Mbegu na Viwatilifu kwa wakati mwafaka

**Mkoa wa simiyu unazalisha asilimia 60 (%) za Pamba yote inayolimwa Nchini na kwa msimu wa mwaka 2021-2022 Mkoa umejiwekea malengo ya kuzalisha tani 500,000 ambapo Wilaya ya Itilima ikiwa na jukumu la kuzalisha tani 70,000 za Pamba.**

.

**HITIMISHO**

Scanned with CamScanner